



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZAMITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU



Tarehe: 06/09/2021


TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA KUKUSANYA MAPATO YATOKANAYO NA MADINI YA UJENZI, USHURU WA KITUO KIDOGO CHA MAGARI MADOGO KISESA NA KITUO KIKUU CHA MABASI MAGU KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DESEMBA KWA MWAKA WA FEDHA 2021-2022

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu anapenda kuwatangazia wananchi wote wa ndani na nje ya wilaya ya Magu wenye sifa na nia ya kufanya kazi ya ajira ya muda kwa nafasi ya kukusanya mapato yatoakanayo na madini ya ujenzi katika maeneo ya Igekemaja, Kitumba, Kanyama, Kisesa, Isangijo, Ihayabuyaga, Welamasonga, Matale, Busekwa, Nyashigwe, Matela, Muda, Kisesa 'B', Lugeye, Bundilya/Kahangara, Ilungu/Nyashimba/Bugabu, Kabila, Mahaha na Ilula, Kituo cha magari madogo Kisesa na kituo cha mabasi makubwa na madogo Magu.

SIFA ZA MWOMBAJI:

1. Awe na hati ya nyumba au wadhamini wawili wenye mali isiyohamishika. dhamana isiyohamishika
2. Mwombaji anatakiwa kuweka kiasi cha fedha kama dhamana (Deposit) kutegemeana na chanzo anachoomba.
3. Mwombaji aonyeshe eneo analoomba kufanyia kazi.
4. Mwombaji aonyeshe uzoefu wa kazi anayoiomba
5. Ataje anuani kamili ya ofisi na mahali ilipo kwa urahisi wa mawasiliano.
6. Atakayepata atatakiwa kuingia mkataba na halmashauri ya Wilaya ya Magu.
7. Mwombaji ataje makadirio ya kiwango atakachokusanya kwa mwezi na kwa mahali husika.
8. Mwombaji atalipia ada ya maombi ya Tzs 50,000/= katika benki NMB akaunti ya Amana iitwayo MDC MISCELLANEOUS DEPOST FUND 31210000950
9. Barua zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo. Juu ya barua ionyeshwe jina la chanzo na mahali kilipo. Barua zote ziwasilishwe kwa Mkurugenzi kwa anwani ifuatayo:-
Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya wilaya ya Magu,
S.L.P 200,
Magu.
10. Barua zote za maombi zitapokelewa katika ofisi ya manunuzi na ugavi iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu.
11. Vigezo vya tathmini ya barua ni kama ilivyoainishwa kwenye tangazo hili.
12. Malipo yatakuwa asilimia 10 ya makusanyo yote kwa mwezi.

13. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni 13/09/2021 siku ya Jumatatu kabla ya saa 5:00 asubuhi. Barua zote zitafunguliwa hadharani mara tu, mbele ya waombaji wa nafasi za kazi au wawakilishi wa waombaji wa nafasi za kazi wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa barua katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Magu.


Fidelica G. Myovela
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
MAGU.

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MAGU.**